[2013]

JAMII ZA WAKUSANYA MATUNDA, WAWINDAJI WA ASILI NA WARINA ASALI

# WASILISHO LA MAONI YA KATIBA MPYA YA JAMII ZA WAWINDAJI, WARINA ASALI NA WAKUSANYA MATUNDA WA ASILI LILILOWASILISHWA KWA TUME YA KURATIBU NA KUKUSANYA MAONI YA KATIBA MWAKA 2013

# MAPENDEKEZO YA MAONI YA KATIBA YA JAMII ZA WAWINDAJI, WARINA ASALI NA WAKUSANYA MATUNDA WA ASILI

Katika wasilisho letu tulipenda kuanza kwa kunukuu maneno ya Rais wa kwanza wa Afrika ya Kusini mwafrika **Mh. Nelson Mandela** alivyosema kwamba;

***"…..A country is not judged by how it treats its highest class citizens but its lowest class citizens…."***

*Tafsiri isiyo rasmi ni kwamba;* ***"Nchi haihukumiwi kwa njinsi inavyo shughulikia watu wake wa daraja la juu bali inavyoshughulikia watu wa daraja la chini"***

## 1.0 UTANGULIZI NA HISTORIA

Jamii za wawindaji wa asili, wakusanya matunda na warina asali wa asili ni kundi la jamii au makabila machache nchini Tanzania ambao bado wanafuata mila na desturi zao za asili. Makabila yaliyopo katika kundi hili kwa sasa ni pamoja na;

- **WAHADZABE**
- **WAAKIYE (Ndorobo)**

Jamii hizi kiasili hujishughulisha na kutegemea rasilimali za asili katika kuendesha mfumo wa maisha kama njia yao rasmi ya kujipatia mahitaji ya msingi ikiwa ni pamoja na malazi, mavazi na chakula. Jamii hizi zinajishughulisha na shughuli zifuatazo;

- **Uwindaji wa asili,**
- **Ukusanyaji wa matunda asili,**
- **Uchimbaji mizizi** ya **asili,**
- **Urinaji wa asali.**

## 2.0 MAKAZI

Jamii hizi zinapatikana katika maeneo yao ya asili ambayo hata kabla ya uhuru walikuwa wakiishi. Hata hivyo ugumu wa maisha na sababu nyinginezo zimesababisha jamii hizi kuhamia sehemu nyingine za nchi na kutawanyika kama njia ya kujitafutia maisha. Hata hivyo mpaka sasa jamii hizi hupatikana katika ukanda wa kaskazini mwa nchi ya Tanzania katika maeneo yafuatayo;

2.1**. Wahadzabe**; hawa wanapatikana katika maeneo yafuatayo;

a. Vijiji vya Domanga, Yaide chini, Mongo wa mono ( Yaeda Valley) katika wilaya ya Mbulu, mkoa wa Manyara ;
b. Kijiji cha Sungu katika wilaya ya Meatu, mkoa wa Simiyu;
c. Kata ya Mang'ola katika wilaya ya Karatu, Mkoa wa Arusha;

d. Kijiji cha Munguli vitongoji vya kikaranga na kipamba wilaya ya Iramba katika mkoa wa Singida

2.2. **Akiye (Ndorobo)**; hawa wanapatikana maeneo yafuatayo;

e. Kijiji cha Kimana kitongoji cha Napilukunya, Kijiji cha Ngapapa katika wilaya ya Kiteto, Mkoa wa Manyara; na,
f. Kijiji cha Kakesio katika wilaya ya Ngorongoro, mkoa wa Arusha.

## 3.0 IDADI YA WATU

Jamii za wawindaji na wakusanya matunda nchini Tanzania kwa idadi ni wachache sana na hii imechangiwa na changamoto mbalimbali ikiwepo magojwa kutokana na kukosa huduma za afya katika maeneo wanamoishi, njaa hususan ukame unapodumu kwa muda mrefu na kusababisha ukosefu wa matunda, asali na wanyama wa kuwinda, vile vile sheria zinazo wanyima kuingia katika mapori kuwinda na kukusanya matunda. Kutona na tafiti mbali mbali jamii ya Wahadzabe wanakadiriwa kuwa kati ya 1000 hadi 1500 (Taarifa ya kikundi kazi ya Kamisheni ya Afrika ya Haki za watu wa asili ya mwaka 2005). Angali Wakiye pia wanakadiriwa kuwa kati ya 300 hadi 500 tu.

## 4.0. MFUMO WA MILA NA DESTURI

Jamii hizi kama ilivyo kwa makabila mengine katika bara la Afrika na kwa Tanzania pia zina mila na desturi zao zenye kuelezea upekee wa jamii hizi kuwa tofauti na jamii nyingine. Mila na desturi za jamii hizi zimewezesha jamii hizi kupambana na mazingira wanamoishi na kukabiliana na changamoto za maisha kama ilivyo kwa jamii nyingine. Kiasili jamii hizi zinafuata mfumo wa mila na desturi ambazo hutegemea mali na rasilimali asili kama wanyama pori, matunda pori, mizizi na asali kama mfumo wao rasmi wa chakula na kipato. Kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani, mila na desturi ya jamii hizi zimekuwa zikionekana kupitwa na wakati hivyo kusahaulika katika mipango na mikakati ya maendeleo ya nchi yetu jambo lililosababisha jamii hizi kuendelea kuonekana kuwa chini na nyuma kimaendeleo, hivyo kushindwa kabisa kushiriki kikamilifu katika mipango ya maendeleo na kutengwa katika mipango ya nchi.

Kule kutengwa katika mipango na mikakati ya maendeleo ya nchi jamii hizi zimejikuta zikiishi sehemu za pembezoni na hivyo kuhitaji uangalizi wa kipekee na upendeleo maalum ili kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia ya nchi, katika mazingira au maeneo wanamoishi, ili waweze kujikwamua na umasikini kiuchumi, kijamii na kisiasa, angali sera na sheria za nchi kama katiba zikilinda mila, desturi, tamaduni na mifumo ya asili ya maisha ya jamii hizi. Jamii hizi kwa miaka mingi wamejisikia **wanyonge waliotengwa (Marginalized)** kwa muda mrefu tangu uhuru**.** Kutokana na kutengwa katika mfumo wa sheria na sera za nchi hususan katiba ya

sasa, sheria ya wanyama pori, misitu, sheria za mazingira, pamoja na sheria za ardhi jamii hizi kwa **uchache wao (Minority)** na hali halisi ya mfumo wa maisha yao wamejisikia hawawezi kujitetea, kudai na kusimamia haki zao za msingi pale zinapokiukwa na sera na sheria zilizotungwa nchini ambazo ni kandamizi na zisizorafiki kabisa na mfumo wa maisha yao.

Jamii hizi kutokana na mila na desturi zao, ni dhahiri kwamba mfumo na aina ya maisha yao, haziendani na mifumo hii ya kisasa-(modernity) hivyo mila na desturi zao zipo katika hatari ya kuonekana hazifai hata kama ni nzuri na hazipingani na sheria za nchi. Vile vile, jamii hizi kutokana na mfumo wao wa maisha na mazingira wanamoishi kutohusishwa na mipango ya maendeleo ya nchi hali ambayo imewafanya watunga sera na wadau wengine kutokuelewa maisha na mifumo yao kikamilifu.

Ni muhimu pia kutambua na kujua kwamba jamii za wawindaji wa asili ni kati ya jamii chache zilizobaki pengine barani Afrika na duniani ambao bado wanaendelea kuishi kwa kushirikana hata katika rasilimali ardhi, hivyo wao wanaendelea na wanapenda kuishi kwa kumiliki kwa pamoja rasilimali zilizopo kwenye maeneo yao na kutumia rasilimali hizi kwa pamoja kama kundi au jamii kwa ujumla na hii ni kutokana na mfumo wao wa maisha (Collective Property Ownership). Mfumo huu wa pamoja ni sehemu kubwa ya maisha, mila, desturi na tamaduni kwa jamii hizi. Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu nchini ni dhahiri kwamba rasilimali zilizopo zisingeweza kutosheleza mahitaji ya kila mtu, hivyo kuwepo kwa makundi kama haya ambayo bado wanamilki rasilimali kwa pamoja ni fursa nzuri kama sheria za nchi zitalinda na kuendeleza aina hii ya umilki wa pamoja. Hata hivyo umiliki huu wa pamoja wa raslimali ndiyo nguzo kuu ya kuendeleza na kuimarisha ujamaa na kujitegemea.

Kwa bahati mbaya sheria na sera za nchi yetu zimejikita zaidi katika kuendeleza na kulinda mfumo wa umilki wa raslimali kwa mtu mmoja mmoja au kwa makundi yaliyosajiliwa kisheria zaidi kuliko kutambua na kulinda mfumo wa jadi wa umilki wa pamoja wa kimaisha kwa jamii hizi.

## 5.0 LUGHA NA TAMADUNI

Kama ilivyo kwa jamii nyingi barani Afrika jamii hizi za Wahadzabe na Akiye wanayo lugha zao na tamaduni ambazo wanawekwa katika kundi la jamii zinazozungumza **lugha ya Khoizan** ambao wanapatikana kusini mwa bara la Afrika hususan nchi za Afrika Kusini na Namibia. Lugha ya jamii hizi hufanana kwani wote wana **Click** katika matamshi yao wakati wa kuzungumza**.**

Hata hivyo jamii hizi pia wanatambuliwa kwa utamaduni wao wa kutumia upinde na mishale kuwinda wanyama pori, kuvaa ngozi za wanyama pori na kula vyakula vya asili. Mfano, katika jamii ya Wahadzabe, wanyama kama nyani na tumbili ni wanyama wazuri ambao huchinjwa wakati wa kuoza au kuoa. Jamii hizi pia kama

ilivyo kwa jamii nyingine hujishughulisha na matendo ya kiutamaduni kama tohara kwa wavulana, matambiko, ndoa za mila na ujenzi wa nyumba wa kipekee kwa kutumia majani.

Jamii hizi pia zina mila na tamaduni nzuri zinazohitaji kutunzwa kulindwa na kuendelezwa kwenye sheria za nchi hususan katiba ya nchi na sheria nyingine. Kwa mfano jamii hizi katika masuala ya kulinda na kuhifadhi mazingira, mila na destruri zao hulazimisha uhifadhi wa mazingira kama kutokuwinda baadhi ya wanyama na kulinda baadhi ya miti isikatwe kwani ina umuhimu kimila na tamaduni zao. Mfano miti ya dawa pamoja na wanyama wanaotumika kama sehemu ya matambiko kama vile Twiga, Ngiri, Swala, Pofu na kadhalika.

Vile vile kwa jamii kama wahadzabe, mwanamke au wanawake wana nguvu katika kufanya maamuzi katika ngazi ya familia kuliko wanaume jambo linalotofautisha jamii hizi na jamii nyingine za kiafrika jinsi zinavyo wachukulia wanawake na nafasi yao katika jamii. Hizi ni baadhi ya mila na desturi nzuri zinazohitaji kuhifadhiwa na kulindwa ili jamii nyingine ziwezekujifunza kutokana na mila na desturi za makundi hayo kuwa mwanamke anao uwezo wa kuwa kiongozi bora katika jamii na katika nchi kwa ujumla.

## 6.0 MGAWANYO WA KAZI

Kama ilivyo kwa jamii nyingine, jamii za wawindaji na wakusanya matunda wanautaratibu wa mila wa mgawanyo wa kazi. Kwa mfano katika jamii hizi, kazi ya wanaume wenye umri zaidi ya miaka 18 wanamajukumu ya kuwinda wanyama na kutoa ulinzi kwa jamii pamoja na kupambana na maadui angali wanawake pamoja na vijana chini ya miaka 18 wanakazi ya kukusanya matunda na kubaki nyumbani kutunza watoto.

## 7.0 MFUMO WA UONGOZI

Jamii hizi ni za kipekee ukilinganisha na jamii nyingine nyingi barani Afrika. Jamii hizi japo zinamila na desturi zao za asili lakini bado hazina mfumo wa uongozi ulio rasmi.

Jamii hizi wao huheshimu na kufuata maelezo kutoka kwa mtu yeyote aliye na umri mkubwa kwa wakati ule ndani ya jamii. Hata hivyo kutokana na kuwa jamii hizi ni za wawindaji, wanautaratibu wa kukaa katika kambi kutokana na upatikanaji wa wanyama na hivyo kutumia kambi hizo kujipangia taratibu na kujadiliana namna ya kukabiliana na changamoto zinazo wakabili na kujigawia kazi bila uongozi wa aina yoyote.

Hivyo basi ni dhahiri kwamba jamii hizi namna yao ya maisha ni tofauti na mfumo huu wa kisasa-modernity wenye kuhimiza au kulazimisha jamii na makundi ya watu kuwa na uongozi wa kuchaguliwa au kuteuliwa. Hivyo basi ni wakati muafaka kwa Sheria na sera za nchi kulinda na kutambua mfumo wa uongozi wa jamii hizi.

## 8.0 SIFA ZA JAMII ZA WAWINDAJI, WAKUSANYA MATUNDA NA WARINA ASALI WA ASILI

- Ni wawindaji wa asili, wanaookota/ kukusanya matunda na wanaorina asali.
- Jamii hizi pia bado zinaishi kwenye bustani ya Aden ambazo sisi tunaita mapori.
- Jamii hizi huwa na mila na desturi zenye kutegemea sana ardhi na mazingira kwa ujumla kama sehemu ya mila, desturi, na matambiko yao.
- Jamii hizi hufanya kazi na kuishi kwa kushirikiana kwa pamoja----collective rights –socialists

## 9.0 HALI YA SASA YA JAMII HIZI

Kwa miaka ya karibuni jamii hizi zimekuwa zikiishi kwa taabu sana, kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi na kukua kwa teknolojia, angali jamii hizi bado wanafuata mfumo wa mila na desturi zao za asili jambo linalowafanya kutengwa (Marginalized). Katika mfumo wa sheria wa nchi yetu kama katika sera na sheria mbalimbali zinazotungwa na bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujumla hazizingatii haki na maslahi ya jamii hizi. Mfano; mpaka sasa hakuna sera au sheria maalum ya nchi yenye kuendeleza ustawi wa jamii hizi ambazo bado zinaishi katika mfumo wa mila na desturi za asili.

Hata hivyo kutokana na ukosefu wa uwakilishi wa jamii asili katika vyombo vya maamuzi kama bunge na serikali jamii hizi zimekuwa za pembezoni zisizoshiriki katika mipango na mikakati ya nchi. Hivyo jamii hizi zinakosa fursa ya kusema na kutoa madai yao ili waweze kusaidiwa na serikali na hii imetokana na kukosekana kwa sera na sheria zinazolinda na kutetea haki na maslahi ya jamii za asili.

Ukosefu wa sera na sheria zinazozingatia maslahi ya jamii hizi, umesababisha jamii hizi kupoteza ardhi kwa njia mbalimbali kama vile; ardhi yao kufanywa hifadhi ya wanyama pori kama ilivyofanywa eneo la Wahadzabe katika wilaya ya Meatu, kijiji cha Sungu kuwa WMA (Wildlife Management Area) mwaka 2011; na ardhi yao kuvamiwa na jamii nyingine hususan wakulima. Kutokana na changamoto hizi jamii hizi zimejikuta zikihangaika kutafuta maeneo ya kuwindia bila mafanikio jambo linalowapelekea kuingia katika hifadhi za wanyama pori ambapo mara nyingi wamekuwa wakijikuta mikononi mwa askari wa wanyama pori- anti-poaching.

Kutokana na kukosekana kwa sheria na sera za nchi zinazolinda na kuendeleza mfumo wa asili kwa jamii hizi, zimekuwa zikididimizwa na kukandamizwa hata wakikutwa wanawinda kwa kujipatia chakula wanakamatwa kama majangili. Sheria ya wanyama pori kwa mfano haitambui kuwa watu wa jamii za asili wanahaki na hutegemea uwindaji wa asili kama sehemu rasmi na mfumo wa chakula kwa jamii hizi.

Kutokana na changamoto hizi zote zinazo kabili jamii hizi za wawindaji na wakusanya matunda, jamii hizi zinadai haki ya kutambuliwa na katiba mpya pamoja na madai mengine. Kwa matinki hiyo basi jamii za wawindaji na wakusanya matunda wanapenda kutoa mapendekezo yao kwa Tume ya Kuratibu na Kukusanya maoni ya wananchi kwa ajili ya kuandika katiba mpya.

## 10.0. MAPENDEKEZO YA JAMII ZA WAWINDAJI, WARINA ASALI NA WAKUSANYA MATUNDA WA ASILI KWA TUME YA KURATIBU NA KUKUSANYA MAONI YA MABADILIKO YA KATIBA TANZANIA

### 10.1 HAKI YA KUTAMBULIWA KIKATIBA NA KISHERIA

10.1.1 **Maelezo;** Tangu historia ya nchi yetu, hakujawahi kuwepo kwa sera, sheria wala katiba ambayo inavipengele vyenye kutambua uwepo wa jamii asili na haki zao nchini Tanzania .Ukosefu huu wa sera, sheria na katiba kutotambua jamii asili imekuwa ndiyo chanzo cha manyanyaso, kubaguliwa, kutengwa, kudharauliwa na kuibiwa rasilimali zao za asili bila ya kunufaika licha ya kuwa waangalizi wa rasilimali hizo. Katiba ya sasa ipo kimya kuhusu jamii hizi tengwa na za asili huku sheria na sera mbalimbali zisizo rafiki zikitungwa bila ya kushirikisha jamii hizi licha ya kuwa waathirika wa kubwa wa sheria na sera hizo. Katiba ya sasa ya Tanzania haitambui mfumo wa uendeshaji wa maisha ya asili (Uwindaji na ukusanyaji matunda) kama mfumo rasmi wa maisha (Livelihood) unaotegemewa na jamii hizi. Vilevile Katiba ya sasa pia haitambui uwepo (existence) wa makundi ya jamii kama hizi nchini hivyo kukosekana kwa ulinzi wa haki za jamii hizi kisheria.

10.1.2 **Pendekezo**; Tunapendekeza katiba mpya kutambua Uwepo wa kundi la jamii asili (Indigenous), jamii tengwa (marginalized) na kundi dogo (Minority) nchini Tanzania lenye kuhitaji upendeleo maalum na uangalizi maalum wa kikatiba, kisheria na kisera kama walivyofanya mataifa mengine kama Kenya katika Ibara ya 56 ya katiba yao, Afrika ya Kusini, Botswana, Cameroon na Chad.

### 10.2 HAKI ZA ARDHI NA RASILIMALI ZA ASILI

10.2.1 **Maelezo**: Haki ya ardhi ni haki ya msingi ya kila binadamu kwa mantiki kuwa hakuna maendeleo bila ya kuwa na ardhi. Hivyo ardhi ni raslimali kuu ambayo ni hitaji kuu la kila binadamu. Katiba ya sasa haina vipengele wazi vinavyohusu wala kuzungumzia ardhi kama rasilimali muhimu sana kwa ustawi wa jamii ya watanzania. Kwa mfano kipengele cha katiba ya sasa

Ibara ya 24 ambayo inazungumzia haki ya kumiliki mali haielezi kinagaubaga kuwa mali inayozungumziwa na kipengele hicho ni pamoja na ardhi. Ukosefu wa vipengele vya ardhi katika katiba inafanya ardhi kuwa si rasilimali muhimu kwa ustawi wa jamii hivyo inakosa ulinzi na uangalizi wa kikatiba. Hata hivyo ukosefu huu, umepelekea sheria mbalimbali zilizotungwa kuwa kichocheo cha ukiukwaji wa haki za jamii za asili, mfano; Sheria za ardhi za mwaka 1999, hazitambui mfumo wa umiliki na utumiaji wa ardhi wa pamoja (collective right over land) ambao ndiyo unao zingatia maslahi na mahitaji ya wawindaji na wakusanya matunda wa asili kwa kuwa mfumo wa maisha w\a kundi la jamii hizi hutegemea zaidi utumiaji wa ardhi na rasilimali nyingine kwa pamoja badala ya ule wa umiliki wa mtu mmoja mmoja.

Ukosefu wa utambuzi wa ardhi kwa matumizi ya uwindaji wa asili umesababisha utungwaji wa sheria zisizo zingatia haki za jamii za wawindaji kama sheria za wanyama pori, misitu, mazingira ambazo zinakataza uwindaji wa asili, uvunaji wa matunda katika mapori urinaji wa asali na uchimbaji mizizi ya asili mpaka kutolewa kwa kibali maalum na mamlaka husika bila kujali kuwa uwindaji ni haki ya msingi wa jamii hii ambayo inategemea kuwinda katika kujipatia chakula. Sheria za wanyama pori pia zimechangia maeneo mengi yanayokaliwa na jamii hizi kupandishwa hadhi kuwa hifadhi au kupewa wawekezaji bila hata kushirikisha jamii hizi hivyo kusababisha kuondolewa kwa nguvu bila kupata fidia ya hasara zinazotokana na usumbufu huo.

10.2.2 **Pendekezo**; Ardhi kuwa ni sehemu ya kikatiba-(constitutional category) faida ya kuweka ardhi kuwa ni sehemu ya kikatiba ni kwanza kuongeza ulizi wa ardhi kama rasilimali muhimu zaidi, lakini pia watanzania watapata fursa ya kusema na kuweka misingi na miongozo ya namna wanavyotaka ardhi yao ilindwe. Kwa kuwa katiba ndiyo sheria pekee yenye kutoa fursa kubwa ya ushiriki wa watanzania ni dhahiri kwamba kama ardhi itawekwa kama sehemu ya katiba ni fursa kwa wantazania katika kuhakikisha ushiriki wao kikamilifu.

10.2.2.1 Katiba pia itambue kwa kutaja makundi ya ardhi kuwa ni pamoja na ardhi ya vijiji na jamii (Community land/collective property), ardhi ya umma na ardhi binafsi. Kwa mantiki hii aina za ardhi tunazopendekeza ni kama ifuatavyo;

- Ardhi ya Umma ni ardhi yoyote ambayo haipo katika mipaka ya vijiji au jamii.
  - Ardhi inayotumika kwa matumizi ya serikali.
  - Ardhi iliyohifadhiwa kwa matumizi maalumu kama vile Hifadhi za taifa, mbuga za wanyama, misitu, barabara,vyanzo vya maji, maziwa ,mito,fukwe, na ardhi nyingine yoyote itakayotengwa kwa makusudi hayo kwa mujibu wa sheria itakayotungwa na Bunge
- Ardhi ya Jamii ni ardhi iyotengwa au kutumiwa na jamii fulani ndani ya ardhi ya kijiji.
- Ardhi ya Binafsi ni ardhi inayomilikiwa na mtu binafsi kwa mjibu wa sheria.
- Ardhi ya Vijiji ni ardhi iliyopo kwenye mipaka ya kijiji na sio ardhi ya jamii .

10.2.2.2 Ardhi ya jamii itumiwe kwa kuzingatia mfumo wa maisha wa jamii husika kwa mfano; kama jamii ni wawindaji, basi ardhi yao itengwe kwa makusudi ya uwindaji wa asili kwa manufaa ya jamii yote na kulindwa na sheria ya Bunge sawa na ardhi ya hifadhi ya wanyama pori na misitu.

10.2.2.3 Kuweka utaratibu maalum wa kuruhusu wawindaji wa asili kuruhusiwa kuwinda kwenye maeneo ya hafadhi hususan nyakati za upungufu wa wanyama katika maeneo yao.

10.2.2.4 Katiba pia itoe haki kwa jamii za wawindaji wa asili ya kutumia na kunufaika na rasilimali zote zinazopatikana katika maeneo yanayokaliwa na jamii za wawindaji na wakusanya matunda na iwapo rasilimali hiyo inafaa kunufaisha watanzania wote, basi katiba itoe haki kwa jamii husika kuwa ndiyo wasimamizi wa rasilimali hiyo na kuwajibika kugawa kiwango cha 50% kuingia katika hazina ya taifa kwa manufaa ya wananchi wote na 50% ibaki kwa manufaa yao.

10.2.2.5 Katiba izuie ubadilishwaji wa ardhi ya vijiji au jamii kuwa hifadhi ya wanyama pori.

## 11 UKOMO WA UMILIKI NA USIMAMIZI WA ARDHI

11.1 **Maelezo**; Katiba ya sasa haielezi kiasi cha ardhi kinachomilikiwa na mtu mmoja hivyo kutoa mwanya kwa wenye uwezo wa kifedha kunyakua, kupora na kuhodhi ardhi kubwa na kuliacha kundi kubwa la wananchi bila ardhi ya kuzalishia mahitaji yao ya msingi. Umiliki huu wa ardhi bila ukomo umekuwa kichocheo kikubwa sana cha migogoro ya ardhi nchini.

**Ufafanuzi zaidi**; Katika suala la umiliki na usimamizi wa ardhi, Katiba ya Jamhuri ya Tanzania ipo kimya hivyo rasilimali muhimu kama ardhi kukosa udhibiti thabiti jambo linalopelekea ukiukwaji mkubwa wa haki za wananchi kwa masuala ya ardhi. Mfano; mgogoro wa mwaka 2007 huko Yaeda Chini kati ya wahadzabe na mwekezaji wa kampuni uwindaji ya kibiashara ya Eshkesh. Hii ni kutokana na suala zima la usimamizi na utoaji wa ardhi kuwa mikononi mwa Rais na hivyo kupelekea Rais kuweza kutoa au kutwaa ardhi bila kupata ridhaa ya wananchi. Mamlaka ya Rais katika ardhi imechochea migogoro mikubwa kati ya wawekezaji na wananchi ambao hawahusishwi katika michakato ya kutoa ardhi zao kwa uwekezaji.

11.2 **Pendekezo**; Hivyo basi, ili kuzuia uwezekano wa utumiaji mbaya wa madaraka kwa Ofisi ya Rais ambaye ndiye mdhamini wa ardhi kwa niaba ya watanzania, katiba mpya iondoe umiliki wa ardhi mikononi mwa Rais badala yake, katiba

11.2.1 Ieleze kuwa ardhi ya Tanzania ni mali ya watanzania wote, kama taifa, kama jamii na kama mtu mmoja mmoja. Pia ardhi itumiwe kwa manufaa ya watanzania wote na itatolewa kwa kuzingatia usawa, uwazi, uzalishaji, uendelevu na kujali hifadhi ya mazingira.

11.2.2 Iundwe **tume ya wajumbe 13** kusimamia na kuratibu utumiaji na umiliki wa ardhi ambao utakuwa ndiyo chombo chenye mamlaka ya mwisho katika kuamua masuala ya ardhi. Upatikanaji wa wajumbe wa tume ya ardhi ufuate utaratibu ufuatao;

11.2.3 , mwakilishi wa wafugaji,

11.2.4 wakulima,

11.2.5 wawindaji wa asili,

11.2.6 mwakilishi kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali,

11.2.7 mwakilishi kutoka vyama vya siasa,

11.2.8 mwakilishi kutoka wizara ya ardhi Tanzania bara

11.2.9 Mwakilishi kutoka wizara ya ardhi Tanzania visiwani,

11.2.10 mwakilishi kutoka baraza la mazingira,

11.2.11 mwakilishi kutoka kundi la wanawake

11.2.12 mwakilishi kutoka kundi la walemavu,

11.2.13 pamoja na wajumbe wengine watatu watakaoteuliwa na waziri wa ardhi kutokana na uzoefu, uadilifu, pamoja na elimu katika masuala ya ardhi.

Namna ya kupatikana kwa wajumbe wanaotokana na makundi tajwa 10 ni makundi husika kupeleka jina mmoja kwa waziri wa ardhi kwa uteuzi.

11.2.13.1 Baada ya wajumbe hao kuteuliwa na waziri wa ardhi, watapelekwa bungeni kwa usaili-(public vetting) kabla ya kupelekwa kwa rais kwa ajili ya kuapishwa.

11.2.13.2 Wajumbe hao Watatumikia Tume kwa kipindi cha miaka 5 na wataweza kuteuliwa tena kwa kipindi cha miaka 5 pekee.

11.2.13.3 Wajumbe hao watawajibika kwa Bunge.

11.2.13.4 Wajumbe hao wa Tume watachagua mwenyekiti na Katibu kutoka miongoni mwao ambao watatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria itakayotungwa na Bunge

11.2.13.5 Mjumbe anaweza kuondolewa kwenye Tume kwa kukosa uadilifu, kwa kushindwa kutimiza wajibu wake kikamilifu, kuchaguliwa kushika nyadhifa nyingine, kufariki dunia au kujiuzulu. Makundi tajwa yanaweza kumbadilisha mwakilishi wao wakati wowote pindi watakapokosa uaminifu naye.

11.2.13.6 Mjumbe anayechaguliwa kuwa mwakilishi wa makundi yaliyotajwa hapo, ataondolewa wakati wowote au saa yoyote pindi itakapobainika na kundi husika kwamba mjumbe ama kwa makusudi au namna yoyote ameacha kutetea maslahi ya kundi husika kwenye Tume.

## 11.3 UKOMO WA ARDHI

11.3.1 Tunapendekeza kuwa ili kuleta usawa katika umiliki na utumiaji wa ardhi kwa wananchi wote tunataka katiba itaje ukomo wa ardhi ambao mtu mmoja anaweza kumiliki. Tunapendekeza Tume ya Taifa ya Ardhi ifanye land audit ili kuratibu ukomo wa umilki wa ardhi kwa watu binafsi .

11.3.2 Tume iangalie na kuzuia umiliki wa ardhi wa mtu mmoja mmoja zaidi ya eneo moja.

11.3.3 Tume ya Ardhi kuratibu soko na uuzaji wa ardhi mjini na vijiji ili kulinda ardhi na haki za watu wanyonge.

11.3.4 Tume kuratibu na kupiga marufuku upanuzi wa mbuga za wanyama pori au hifadhi kwani upanuzi huo huchukua ardhi za wananchi na kuchochea migogoro baina ya wananchi na mamlaka za hifadhi ya wanyama pori.

## 12 HAKI YA MAKUNDI MAALUM (MAKUNDI YA JAMII ASILI, JAMII TENGWA NA MAKUNDI MADOGO)

12.1 **Maelezo**; Katiba ya sasa ipo kimya katika kuelezea haki ya makundi maalum ambayo kwa miaka mingi wamesahaulika na kuachwa nyuma kimaendeleo. Makundi haya yanajumlisha jamii za asili kama wawindaji na wakusaya matunda wa asili (Akiye na Hadzabe),

12.2 **Pendekezo**; Kundi la wawindaji na wakusanya matunda wa asili tunapendekeza haki hii iwekwe katika katiba na kubainisha yafuatayo;

12.2.1 Kuwepo fursa ya pekee itakayo patikana kwa ajili ya kutoa upendeleo wa pekee kwa jamii za wawindaji na wakusanya matunda kuwa na **uwakilishi na ushiriki** wao katika vyombo vya maamuzi vya serikali;

12.2.2 Upendeleo katika utoaji wa ajira;

12.2.3 Upedeleo katika utoaji wa huduma za jamii kama elimu, afya, maji n.k;

12.2.4 Kuwezeshwa katika maendeleo ya mila na tamaduni zao;

12.2.5 Haki ya kupata miundo mbinu ya barabara na huduma nyinginezo muhimu.

## 13 HAKI YA UTAMADUNI

13.1 **Maelezo**; Utamaduni ni haki ya msingi ya kila jamii hivyo ni suala la msingi kuzingatiwa katika utungwaji wa katiba ili kulinda utamaduni wa mtanzania kwa manufaa ya taifa na vizazi vijavyo.

13.2 **Pendekezo**; Kwa kuwa utamaduni ni haki ya kila mtu katika jamii, katiba iwe na vipengele vyenye kueleza kuwa;

13.2.1 Kila mtu anayohaki ya kutumia lugha na kushiriki katika utamaduni anaouchagua mwenyewe. Hii itatoa uhuru wa kila mtu kufuata utamaduni anaoupenda.

13.2.2 Kila mtu kuwa na haki ya kutumia lugha yake bila ya kuingiliwa na mtu mwingine;

13.2.3 Katiba izuie na kukataza utumiaji mbaya wa utamaduni wa watu wengine bila kupata ridhaa ya jamii husika. Mfano, yapo makampuni mengi ya utalii na biashara yanatumia utamaduni wa kimaasai kutangaza biashara zao bila kuwanufaisha wamasai. Hoteli nyingi zina sanamu na picha za wamasai bila hata kupeleka huduma za jamii kwa hao wanaowatumia kutangaza biashara zao.

## 14 UTAMBUZI WA UONGOZI WA MILA

14.1 **Maelezo;** Kabla na baada ya ukoloni, Waafrika walikuwa na mfumo wao wa uongozi wa mila ambao uliheshimiwa na jamii za wakati ule. Uongozi wa mila ulionekana kuwa ni uongozi bora na ulisimamia sio tu masuala ya utamaduni bali pia ni uongozi uliojishughulisha na usimamizi wa umiliki na utumiaji wa ardhi pamoja na rasilimali nyingine zilizopatikana katika eneo la jamii hiyo. Uongozi wa mila ulitumika tu kwa jamii husika na haukuweza kuvuka mipaka na kuingilia uongozi wa jamii nyingine. Zipo shughuli ambazo wakati wa ukoloni uongozi wa mila ulijishughulisha ikiwa ni pamoja na kusimamia utatuzi wa migogoro ya aina yote hususan, ndoa, ardhi na migogoro ya kijamii.

14.2 Kwa jamii ya Kihadzabe mfumo wa uongozi haupo kama wa jamii nyingine. Kwa maneno mengine ni kuwa Wahadzabe hawana mtu anayetambuliwa kama kiongozi badala yake wanatumia wazee wenye umri mkubwa kuwa ndiyo viongozi wa kambi ambao kazi yao kubwa ni kuongoza kambi na kutatua migogoro yoyote itakayo ibuka katika kambi zao. Migogoro mikubwa inayoikumba jamii ya kihadzabe ni migogoro ya mila na desturi na migogoro ya ndoa. Hivyo kazi kubwa ya wazee wanaoongoza kambi ni kutatua migogoro ya ndoa kabla ya kufika mahakamani. Katiba ikitambua uongozi wa mila hizi itawezesha jamii nyingi kutatua migogoro kwa njia isiyo ya gharama na ambayo itaendeleza undugu na upendo kwa pande zinazohusika katika mgogoro ili kuifanya kuwa njia mbadala ya kutatua migogoro (Alternative dispute resolution (ADR).

14.3 **Pendekezo;** Katiba mpya itambue uongozi wa mila kama mfumo rasmi wa uongozi unaofuata misingi ya mila na desturi ya jamii husika katika usimamizi wa rasilimali asili na ardhi pamoja na utatuzi wa migogoro inayotokana na utumiaji wa ardhi na rasilimali nyingine za asili . Mfumo huu uwe katika mfumo wa uongozi katika ngazi ya vijiji ambao utakuwa juu ya serikali za vijiji na utajulikana kama BARAZA LA WAZEE WA MILA ambao maamuzi yake yaweza tu kupingwa na kujadiliwa katika mkutano mkuu wa wananchi wote utakao itishwa kwa ajili ya kujadili rufaa iliyotoka na mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa baraza la wazee au la viongozi wa mila katika utatuzi wa migogoro au uamuzi kuhusu jambo lingine lolote katika jamii husika.

Mifano ya utambuzi wa uongozi wa mila kutoka nchi nyingine kama Ghana ni mfano mzuri wa kuigwa kama ilivyo katika katiba yao.

39 (1) Subject to clause (2) of this article, the State shall take steps to encourage the integration of appropriate customary values into the fabric of national life through formal and informal education and the conscious introduction of cultural dimensions to relevant aspects of national planning.

(2) The State shall ensure that appropriate customary and cultural values are adapted and developed as an integral part of the growing needs of the society as a whole; and in particular that traditional practices which are injurious to the health and well-being of the person of the person are abolished.

## 5.0 HAKI YA HATI MILIKI

15.1 **Maelezo;** Haki ya hati miliki ni haki kama ilivyo haki nyingine kwa mantiki kuwa kila mtu binafsi au jamii wanayohaki ya kunufaika na kazi zao zinazohusisha ubunifu, uvumbuzi, fasihi, kazi za sanaa, alama, majina na michoro inayotumika kwenye biashara. Hati miliki inahusisha kazi za sanaa kama vile michoro, picha, sanaa za kuchongwa na usanifu wa majengo.

Haki ya hati miliki inahaki ya kulindwa na sheria ikiwa ni pamoja na Katiba kama ilivyo kwa haki nyingine za binadamu. Haki ya hati miliki Ulimwenguni inalindwa na kifungu cha 27 cha Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu. Tamko hili la ulimwengu linataka mwanadamu apewe ulinzi wa KIMASLAHI na MAADILI kwa ubunifu au ugunduzi wa kitu chochote iwe cha kisayansi, sanaa au fasihi. Katika nchi yetu haki ya hati miliki imetambuliwa katika sheria mbalimbali kama sheria ya ubunifu (Patent Act), Copy rights Act na sheria ya alama za biashara (Trade Mark Act). Lakini pamoja na kuwepo kwa sheria hizi bado jamii za wawindaji na wafugaji hawanufaiki ipasavyo na sanaa, picha na ubunifu wao wa kiutamaduni ambao unatumika kibiashara ndani na nje ya Tanzania. Kwa mfano; yapo matangazo mbalimbali yanayoonyesha utamaduni wa Kimaasai au Kihadzabe lakini jamii hainufaiki na chochote.

Haki ya hati miliki ni muhimu sana kulindwa kwa manufaa na ustawi wa jamii husika na umuhimu huu ulitambuliwa kwa mara ya kwanza kwenye makubaliano ya Mkataba wa Paris kuhusu Ulinzi na Mali za Kiubunifi wa mwaka 1883 na Makubaliano ya Berne kuhusu Ulinzi wa kazi za Uandishi na usanii ya mwaka 1886.

15.2 **Pendekezo**; Tunapendekeza kuwa;

(i) Katiba itambue haki ya hati miliki bunifu kama moja wapo ya haki za binadamu zinazoheshimiwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) Kuwepo na Baraza au Tume ya kuratibu na kusimamia hati ya haki miliki bunifu ili kuzuia wizi wa ubunifu wa jamii za asili na kuweka utaratibu utakao nufaisha jamii husika.

(iii) Kuanzishwe mfuko maalum ambao utakuwa unachangiwa na watumiaji wa hati miliki bunifu za jamii za wawindaji na wakusanya matunda wa asili na wafugaji kama njia ya jamii hizo kunufaika na sanaa za utamaduni wao unaotumika kibiashara.

(iv) Kuzuia utumiaji wa haki ya hati miliki ya jamii hizi za wawindaji na wakusanya matunda wa asili bila ridhaa yao.

(v) Kwa suala la uwekezaji na miradi mingine ya serikali katika maeneo yanayomilikiwa na jamii ni budi kwa katiba ya nchi kuweka vipengele vya kulazimisha kufuata misingi ya kidemokrasia, uadilifu na ushirika mpana na wa kikamilifu kwa jamii husika (Free Prior informed consent).

## 16. HITIMISHO

Kutokana na sababu zilizotajwa hapo juu, kundi hili la wawindaji wa asili, wakusanya matunda na warina asali, ni dhahiri kwamba mfumo wao wa maisha hauendani na mfumo wa kisasa, kama vile mfumo wa vijiji kama njia ya kulinda rasilimali zao kama jamii.

Pia kutokana na idadi ya namba ya jamii hizi kuwa ni chache sana kiasi cha kutishia kupotea katika uso wa dunia, ni dhahiri pia kwamba jamii hii bado zinaishi katika maeneo ya pembezoni hivyo basi ni rahisi kukosa fursa za kimaisha kama mipango maalum haitabuniwa na kupewa umaalum wake unaostahili. Hivyo basi, ni dhahiri juhudi za makusudi zinahitaji zichukuliwe kuhahikisha katiba mpya inatoa fursa maalum kwa makundi haya.